AckySHINE.com

# Je, watu wote wenye virusi vya UKIMWI watapata UKIMWI? Na kama ndiyo, itachukua muda gani?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo, baada ya muda fulani karibia watu wote wenye maambukizi ya Virusi vya UKIMWI wataanza kuugua UKIMWI. Lakini muda kati ya kuambukizwa na kuanza kuugua UKIMWI unatofautiana. Wengine wanaishi muda mrefu. Kwa wastani watu wazee wazima wanaendelea kuishi miaka kumi kabla ya kupata dalili za awali. Watoto wanaopata virusi kabla ya umri wa miaka mitano kwa wastani wanendelea kuishi mwaka moja hadi mitatu. Hakuna jibu la ujumla ni miaka mingapi ataishi tena mtu aliyeambukizwa na virusi vya UKIMWI. Idadi ya miaka ya kuishi baada ya kuambukizwa i inategemea vitu vingi, kinga asilia i inayomkinga mtu, hali ya lishe ya mtu, wakati muafaka na usahihi katika kutibu magonjwa nyemelezi na wakati muafaka na usahihi wa kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kwa Kiingereza Anti-Retro-Viral drugs (ARVS )